

## **KiSwahili non-technical summary of Gogarten, Jacob et al. (*Accepted*) Biotropica**

Idadi ya wanyama katika kundi inaweza kubadilisha ikolojia na jamii yao. Tulitaka kujua mabadiliko ya aina saba ya nyani katika hifadhi ya taifa Kibale, Uganda kuanzia mwaka 1996-2011. Tulihasabu ukubwa wa makundi ya nyani katika hifadhi na msitu uliokatwa na isuokatwa. Pia tulitaka kufahamu kama chakula kinacholiwa na nyani kinaelezea ukubwa wa kundi na mabadiliko ya ukubwa wa aina ya miti katika maeneo ya misitu isiyokatwa kuanzia 1990 mpaka 2013. Hakuna mabadiliko katika ukubwa wa makundi isipo kuwa mbega wekundu (*Procolobusrufomitratus*) ambao: waliongezeka kwa kawaida. Ukubwa wa makundi ya mangabey (*Lophocebusalbigena*) iliongezeka katika msitu usiokatwa, lakini hakuwawa na wanyama wengi na ongezeko lilikuwa dogo. Kwa miaka kadhaa idadi ya wanyama imekuwa ikihesabiwa katika makundi mbalimbali ya nyani wasio ogopa watafiti: makundi matatu ya nyani wenye mkia mwekundu (*Cercopithecusascanius*), makundi nane ya mbega wenye weusi na weupe (*Colobusguereza*) na kundi moja la mbega wekundu. Kundi la mbega wekundu liliongezeka mara mbili kwa ukubwa lakini makundi ya nyani wenye mkia mwekundu na mbega wenye weusi na weupe hayakubadilika (kama matokeo ya jumla). Kwa ujumla, chakula cha tumbili katika msitu usiokatwa kiliongezeka kwa muda lakini ongezeko lilitofautiana kwa kila aina ya nyani. Kufahamu kwa nini makundi ya mbega wekundu yanakuwa makubwa wakati makundi ya nyani wengine hayawi makubwa, tulijadili madhara ya magonjwa na wanyama wanaokula nyama. Tunafikiri mabadiliko katika chakula yanaweza kuwa muhimu zaidi. Ni vigumu kuelewa ikolojia changamani ya kibale, hivyo utafiti zaidi unaitajika katika siku zijazo.

*[Asante kwa ajili ya Wildlife Conservation Society (Tanzania), hasa Tim Davenport, kwa msaada na tafsiri.]*